**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

TANZANIA
COOPERATIVE DEVELOPMENT COMMISSION
Together We Build Our Economy

# *MWONGOZO WA UHAMASISHAJI NA UANZISHWAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA*

***IMEANDALIWA NA:***
TUME YA MAENDELEO YA
USHIRIKA S. L. P 201,
DODOMA.

**JULAI 2021** ***TOLEO LA KWANZA***

YALIYOMO

DIBAJI ........ 1
2.0 WALENGWA NA MADHUMUNI YA MWONGOZO ........ 4
2.1 WALENGWA WA MWONGOZO ........ 4
2.2 LENGO NA MADHUMUNI YA MWOGOZO ........ 4
3.0 UHAMASISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA ........ 5
3.1 Mambo ya kuzingatia kabla ya kufanya uhamasishaji ........ 5
3.1.1 Sifa za mhamasishaji ........ 5
3.1.2 Kutambua mahitaji kwa kuzingatia Mazingira husika ........ 6
3.1.3 Kuandaa Mada/Somo linalokusudiwa kutolewa au kufundishwa ........ 6
3.1.4 Njia za kufanya uhamasishaji ........ 6
3.2 Hatua muhimu za kuzingatia wakati wa uhamasishaji ........ 6
3.3 Hatua muhimu za kuzingatia wakati wa uanzishaji wa Chama cha Ushirika ........ 7
3.3.1 Kufanya uamuzi wa hiari ........ 7
3.3.2 Kuitisha na kufanya Mkutano Mkuu wa Awali ........ 7
3.3.3 Mkutano wa kujadili mapendekezo ya Kamati Anzilishi ........ 8
3.3.4 Kuwasilisha maombi ya kuandikisha Chama ........ 9
3.3.5 Mkutano Mkuu wa kwanza baada ya Chama kuandikishwa ........ 9
3.3.6 Taratibu za Uchaguzi wa Bodi ........ 9
3.4 Uhamasishaji wa Vyama sinzia ........ 10
3.6 Uendelezaji wa vyama vya Ushirika. ........ 10
Umiliki wa Wanachama ........ 10
Udhibiti wa Wanachama ........ 11
Ushiriki wa Wanachama ........ 11
SEHEMU YA NNE ........ 12
5.0 HITIMISHO ........ 12
VIAMBATISHO ........ 13

## DIBAJI

Historia ya Vyama vya Ushirika nchini ilianza kabla ya Uhuru wa Tanganyika ambapo Ushirika wa mazao ya kilimo ulikuwa wa kwanza kuanzishwa. Shabaha kuu ya kuanzisha Vyama hivyo ni kuondoa unyonyaji wa wafanyabiashara ambao walikuwa wakinunua mazao hayo kwa bei ya chini na kuyauza kwa bei ya juu. Kumbukumbu mbalimbali zinaonesha baadhi ya mafanikio ya Vyama vya Ushirika ni pamoja na uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao, majengo, viwanja, mashamba makubwa, na zana za kilimo.

Kutokana na mafanikio hayo, Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali viliweza kuanzishwa katika maeneo mengi nchini kama nyenzo ya kupambana na umaskini na unyonyaji. Katika jitihada za kutatua changamoto hizo, mabadiliko mbalimbali ya Kisheria na Kimuundo yalifanyika na kusababisha kutungwa kwa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ambayo imeanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Sheria hii imeipa Tume jukumu la kuhamasisha na kusimamia maendeleo ya Ushirika nchini kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wakiwemo Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Katika kuhakikisha uhamasishaji unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa Mwongozo wenye lengo la kuwapatia wahamasishaji uelewa wa pamoja kuhusu namna nzuri ya kuhamasisha na kuanzisha Vyama vya Ushirika nchini.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake, ili kuhakikisha majukumu ya uhamasishaji yanatekelezwa ipasavyo kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau mbalimbali.

Ni matarajio ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuwa Mwongozo huu utarahisisha kazi ya kuratibu majukumu ya Uhamasishaji na Usimamizi yanayotekelezwa na Wadau mbalimbali nchini. Aidha, watumiaji wanatakiwa kufanya rejea katika Mwongozo huu ili kuhakikisha kwamba, Vyama vya Ushirika vinaanzishwa na kuendeleshwa kwa kuzingatia taratibu kama zilivyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika. Hii itawezesha uwepo wa Vyama vya Ushirika imara na endelevu na vinavyojibu mahitaji ya

wanachama wake na jamii kwa ujumla katika masuala ya kiuchumi na kijamii.

Dkt. Benson O. Ndiege

**<u>MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA</u>**

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali inatambua kuwa Ushirika ni njia moja wapo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi hususani wakulima, wafanyabiashara wadogo wadogo na wananchi kwa ujumla. Aidha, licha ya changamoto zinazovikabili Vyama vya Ushirika bado Vyama hivyo vimeendelea kutoa huduma kwa wanachama na jamii kwa ujumla. Hivyo, ili kuondokana na changamoto hizo, mabadiliko mbalimbali ya kisheria na kimuundo yalifanyika na kusababisha kutungwa kwa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ambayo imeanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Sheria hii imeipa Tume jukumu la kuhamasisha na kusimamia maendeleo ya Ushirika nchini kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wakiwemo Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Sheria ya Vyama vya Ushirika imejielekeza katika kuimarisha Sekta ndogo ya Ushirika nchini kwa lengo la kujenga Vyama vya Ushirika imara, endelevu na vyenye uwezo wa kikidhi mahitaji ya wanachama kiuchumi na kijamii kwenye mazingira ya uchumi wa soko huru. Ili kuhakikisha Ushirika unachangia katika ukuaji wa uchumi, zinahitajika jitihada zaidi za uhamasishaji na ushirikiano miongoni mwaka Wadau mbalimbali kwa lengo la kuanzisha, kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika nchini. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 14 & 15 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 imeelekeza Wizara za Kisekta kuwa na dawati la Ushirika sambamba na kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Ushirika kwa lengo la kuhamasisha uwepo wa Vyama vya Ushirika katika sekta zao.

Kutokana na changamoto ya uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya Ushirika bila kufuata taratibu kama zilizoainishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake imesababisha Vyama hivyo kutokuwa imara na endelevu. Hali hii, imesababisha uwepo wa Vyama vya Ushirika ambavyo sio imara na endelevu. Hivyo, ili kuhakikisha kuwa uhamasishaji unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa Mwongozo wenye lengo la kuwapatia wahamasishaji uelewa wa pamoja kuhusu namna nzuri ya kutekeleza majukumu yao ili kuondoa changamoto za uhamasishaji na uanzishaji wa Ushirika.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 WALENGWA NA MADHUMUNI YA MWONGOZO

Ili kuhakikisha kuwa dhana ya Ushirika inatekelezwa kikamilifu, mwongozo huu umelenga kufikisha kwa Wadau na jamii kwa ujumla maelekezo ya namna ya kuhamasisha maendeleo ya ushirika nchini. Aidha, madhumuni ya mwongozo ni kuwapatia wahamasishaji uelewa na pamoja kuhusu namna nzuri ya kuratibu, kuhamasisha na kuanzisha Vyama vya Ushirika.

## 2.1 WALENGWA WA MWONGOZO

Walengwa wa mwongozo huu ni pamoja na:

- i) Maafisa Ushirika;
- ii) Wizara za kisekta;
- iii) Taasisi mbalimbali, mfano; MoCU, COASCO na BOT
- iv) TFC, SCCULT, VYAMA VYA UPILI na MIRADI ya PAMOJA.
- v) Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi) Kamati za elimu za Mikoa na Taifa;
- vii) Sekretarieti za Mikoa;
- viii) Wadau wengine.

## 2.2 LENGO NA MADHUMUNI YA MWOGOZO

LENGO: Kuweka utaratibu maalum unaopaswa kuzingatiwa na wahamasishaji wote katika kutekeleza majukumu yao ya uhamasishaji na uanzishwaji wa Vyama vya ushirika nchini.

Aidha, madhumuni mengine ya mwongozo huu ni pamoja na:

- i) Kuweka uelewa wa pamoja juu ya dhana ya Ushirika na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika;
- ii) Kuwezesha wahamasishaji kuzingatia taratibu za uanzishaji na usajili wa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake;
- iii) Kuwezesha wahamasishaji kutumia mbinu mbalimbali za kuhamasisha jamii kuanzisha na kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika vilivyopo; na
- iv) Kurahisisha kazi ya uratibu wa majukumu ya uhamasishaji ili kutoa maelekezo na maamuzi yanayofanana kwa Vyama vyote vya Ushirika nchini.

# 3.0 UHAMASISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA.

## 3.1 Mambo ya kuzingatia kabla ya kufanya uhamasishaji

Mambo ya kuzingatia kabla ya kufanya uhamasishaji ni pamoja na:

- Kuwepo kwa Mhamasishaji
- Kubaini wahamasishwaji na mazingira yao
- Kuwepo kwa mada/Somo la uhamasishaji
- Kubaini njia itakayotumika katika uhamasishaji
- Uzingatiaji wa itifaki

### 3.1.1 Sifa za mhamasishaji

Ili kuhakikisha kuwa lengo la Mhamasishaji linatimia kwa kuwa na matokeo chanya, pamoja na sifa nyinginezo, Mhamasishaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

i. Uelewa wa masula ya kiushirika kwa ujumla ***(Kiambatisho Na. 1)***
ii. Awe na uwezo kushawishi watu/jamii anayoihamasisha ili ikubaliane na kufuata yale yaliyokusudiwa;
iii. Anatakiwa kujitahidi kusoma mawazo ya watu wa rika zote ili kufikisha ujumbe kwa hoja zenye mvuto chanya unaoweza kubadili misimamo yao;
iv. Awe na uelewa juu ya somo analohamasisha ili aweze kujenga hoja kwa wasikilizaji;
v. Awe ni mtu anayekubaliana na changamoto zinazoibuliwa/tolewa na wahamasishwaji na kuzitolea maelezo baada ya majadiliano;
vi. Awe na mtazamo chanya kuhusu jambo analotaka kuhamasisha pamoja na jamii husika;
vii. Awe na taarifa za ukweli na uhakika na kutoa ahadi zinzaotekelezeka;
viii. Awe na uelewa na mazingira pamoja na watu/jamii anayoenda kuhamasisha;
ix. Awe na uwezo wa kujibu hoja/maswali kutoka kwa jamii inayohamasishwa;
x. Awe rafiki wa jamii anayotaka kuihamasisha;

xi. Awe na ratiba kwa ajili ya kazi husika ikiwa ni pamoja na kujua muda wa eneo litakalotumika kwa ajili ya uhamasishaji;
xii. Awe nadhifu, msikilizaji makini na mwenye uwezo wa kutumia lugha fasaha; na
xiii. Awe mfuatiliaji ili kujua matokeo ya uhamasishaji alioufanya.

### 3.1.2 Kutambua mahitaji kwa kuzingatia Mazingira husika

Mhamasishaji kabla ya kwenda kwenye zoezi la uhamasishaji, anapaswa kuelewa mazingira ya sehemu husika na aina ya watu anaokwenda kuwahamasisha ili kuwezesha kutoa elimu stahiki yenye matokeo chanya kwa lengo la kuwa na Ushirika imara na endelevu unaojibu mahitaji ya wananchi kwa kuzingatia shughuli za kiuchumi walizonazo.

### 3.1.3 Kuandaa Mada/Somo linalokusudiwa kutolewa au kufundishwa

Mhamasishaji anapaswa kuandaa mada/somo analolikusudia kulitoa/kufundisha kwa wananchi wa eneo/chama husika. Mada hiyo inapaswa kuandaliwa mapema na kwa ufanisi ili kuhakikisha kunakuwepo na matokeo chanya. Mhamasishaji anapaswa kuwa na mwelekeo kwa kuzingatia aina ya Ushirika unatarajiwa kuanzishwa **(Kiambatisho Na. 2)** kwa mujibu wa Sheriana Kanuni za Ushirika.

### 3.1.4 Njia za kufanya uhamasishaji

Ili kuwezesha uhamasishaji kutolewa ipasavyo, Mhamasishaji anatakiwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

i. Vipeperushi;
ii. Mihadhara na mikutano;
iii. Majadiliano kwenye vikundi;
iv. Kisa mkasa (Case study);
v. Ziara ya mafunzo;
vi. Mitandao ya kijamii;
vii. Vyombo vya habari;

## 3.2 Hatua muhimu za kuzingatia wakati wa uhamasishaji

Uhamasishaji hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Kifungu cha 8 (b) kwa lengo la kuwa na Vyama vya

Ushirika imara na endelevu. Uhamasishaji unaweza kufanyika kwa kuzingatia mahitaji ya jamii husika ambapo:

i. Mhamasishaji anaweza kuangalia fursa zilizopo na kuwashawishi wananchi juu ya uanzishwaji wa chama cha Ushirika; na
ii. Wananchi kwa hiari yao wenyewe waone umuhimu wa kuanzisha Chama cha Ushirika.

### 3.3 Hatua muhimu za kuzingatia wakati wa uanzishaji wa Chama cha Ushirika

Hatua za uanzishwaji wa Chama cha Ushirika hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 20 pamoja na Kanuni zake *(Kanuni ya 4-7 & 12).* Mchakato wa kuunda Chama unapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

#### 3.3.1 Kufanya uamuzi wa hiari

Watu wanaokusudia kuanzisha chama cha Ushirika watapaswa kufanya uamuzi wao kwa hiari. Wakishafanya uamuzi huo, watatoa taarifa kwa Afisa Ushirika wa eneo husika ili aweze kukutana nao na kuwapatia mwongozo/maelekezo ya mchakato wa namna ya uanzishaji wa chama cha Ushirika wanachokusudia kuanzisha. Baada ya Mhamasishaji kutoa elimu ya Ushirika hana budi kuwapa muda wananchi ili watafakari kuhusu maamuzi ya aina ya ushirika watakaoweza/wanaotaka kuanzisha kutegemeana na mahitaji yao na mazingira yanayowazunguka.

#### 3.3.2 Kuitisha na kufanya Mkutano Mkuu wa Awali

Mkutano Mkuu wa awali utafanywa chini ya usimamizi wa Afisa Ushirika Mhamasishaji ili kuchagua Kamati anzilishi ambapo miongoni mwao Mwenyekiti na Katibu watachaguliwa. Kazi ya Afisa Ushirika Mhamasishaji itakuwa ni:

i. Kuwaelimisha wananchi wanaokusudia kuanzisha Chama cha Ushirika kuhusu dhana ya Ushirika, taratibu na kazi za kufanya ili kufanikisha uanzishaji wa Chama cha Ushirika;
ii. Mkutano wa Uanzilishi utachagua Kamati ya uanzilishi yenye idadi ya wajumbe kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika; na

iii. Mkutano huu utakasimu madaraka kwa Kamati Anzilishi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yatakayowezesha kuandikishwa kwa chama.

Majukumu ya Kamati anzilishi ni pamoja na;

i. Kujadili kwa kina nia na madhumuni ya chama kinachotarajiwa kuanzishwa;
ii. Kuandaa orodha ya wanachama na mtaji kwa kuzingatia maazimio ya Mkutano wa Wanachama na kuandaa Masharti ya Chama kwa kuzingatia maelekezo kutoka kwa Afisa Mhamasishaji/Afisa Ushirika;
iii. Kuitisha Mkutano Mkuu wa Uanzilishi;
iv. Kutayarisha taarifa ya uwezo wa kiuchumi wa Chama (kidadisi uchumi).
v. Kuandaa Mpango Biashara wa Chama;
vi. Kuandaa makisio ya Mapato na Matumizi (bajeti) ya Chama ya mwaka wa kwanza;
vii. Kuhamasisha wananchi wengine kujiunga na Chama hicho tarajiwa, kupokea viingilio, kupokea fedha za his ana michango mingine kulinana na mahitaji ya Chama kama ilivyokubalika kwenye Mkutano wa uanzilishi;
viii. Kuandaa ofisi ya Chama pamoja na kununua vitendea kazi;
ix. Kufanya mambo mengine yoyote yatakayowezesha kufanikisha mahitaji ya usajili wa Chama kama itakavyoshauriwa na Afisa Uhamasishaji/AfisaUshirika.

### 3.3.3 Mkutano wa kujadili mapendekezo ya Kamati Anzilishi

Baada ya Kamati anzilishi kukamilisha maandalizi yake, kamati hiyo itaitisha Mkutano wa wananchama waanzilishi kujadili mapendekezo yaliyoandaliwa na Kamati. Mkutano utasimamiwa na Afisa Mhamasishaji au Afisa Ushirika yeyote atakayekuwa ameteuliwa na Mrajis na utafanya kazi zifuatazo: -

i. Kuweka utaratibu wa kuchagua Mwenyekiti na Katibu wa kamati anzilishi;
ii. Kupokea taarifa ya kamati anzilishi;
iii. Kukubaliana jina la chama;
iv. Kujadili rasimu ya masharti ya chama na kuyapitisha;
v. Kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya chama;
vi. Kupitisha taarifa ya uwezo wa kiuchumi wa chama (kidadisi uchumi);
vii. Kupitisha mpango biashara wa chama;

viii. Kupitisha Azimio la Maombi ya kuandikisha Chama; na
ix. Kuwapatia kamati anzilishi kazi ya kukamilisha nyaraka muhimu kwa Mrajis.

### 3.3.4 Kuwasilisha maombi ya kuandikisha Chama

Maombi ya kuandikishwa kwa chama cha ushirika yatawasilishwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa kutumia fomu maalum iliyoandaliwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Kifungu cha 32, Mrajis anapaswa kusajili au kutoa sababu ya kutokusajili chama husika ndani ya siku sitini (60) toka maombi ya kuandikishwa kwa chama kuwasilishwa ofisini kwake. Fomu ya maombi ya kuandikishwa chama itafungashwa pamoja nan akala za kumbukumbu zifuatazo:

i. Masharti ya chama – Nakala nne;
ii. Taarifa ya uwezo ya kiuchumi wa chama (kidadisi uchumi) – Nakala nnne;
iii. Makisio ya Mapato na Matumizi – Nakala nne; na
iv. Mihtasari ya Mikutano Mikuu miwili – Nakala nne.

### 3.3.5 Mkutano Mkuu wa kwanza baada ya Chama kuandikishwa

Mkutano Mkuu wa kwanza utahudhuriwa na Wanachama waanzilishi ambao watakuwa wamelipa Hisa na Kiingilio. Mkutano huu utafanya mambo yafuatayo:-

i. Kuchagua Bodi ya Uongozi wa Chama ambayo itakuwa na wajumbe kulingana na sheria ya Vyama vya Ushirika iliyopo na kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo;
ii. Chama kukabidhiwa Hati ya kuandikishwa;
iii. Kupokea maagizo/maelekezo ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika juu ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika uaendeshaji wa chama ; na
iv. Kuweka mikakati ya kutekeleza madhumuni (malengo) ya Chama kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Masharti na Mpango biashara.

### 3.3.6 Taratibu za Uchaguzi wa Bodi

Uchaguzi wa Bodi utafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika. Bodi Anzilishi, kabla ya kuitisha Mkutano Mkuu wa kwanza itatoa tangazo la kuwafahamisha wananchama wanaotaka kuomba uongozi kuchukua fomu za kuomba uongozi katika Chama.

Tangazo hilo litatolewa si chini ya siku 21 kabla ya uchaguzi huo kufanyika. Fomu zilizojazwa zitawasilishwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi (ambaye huteuliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika). Msimamizi wa uchaguziataunda Kamati ya watu waadilifu kuchambua maombi ya wagombea wanaoomba uongozi kwa mujibu wa Kanuni ya 48 (4).

Msimamizi wa uchaguzi atawasilisha majina ya wagombea waliopitishwa na Kamati ya Uchaguzi kwenye Mkutano Mkuu wa kwanza kwa ajili ya kupigiwa kura za siri. Uchaguzi huo wa Bodi ya uongozi ukishakamilika, Chama hutambuliwa rasmi na kuanza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika kwa manufaa ya Wanachama wake na jamii.

### 3.4 Uhamasishaji wa Vyama sinzia.

Endapo kuna uwepo wa Vyama vya Ushirika ambavyo ni sinzia, Mhamasishaji anapaswa kuweka mpango kazi wa jinsi ya kuamsha Vyama sinzia ili viweze kuendelea na malengo ya kuandikishwa kwao. Utaratibu huo unahitaji mhamasishaji kufnaya uchambuzi ili kujua sababu za chama husika kuwa sinzia na kupanga mikakati ya kuamsha chama husika au kuangalia njinsi ya kuunganisha vyama kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake.

### 3.6 Uendelezaji wa vyama vya Ushirika.

Mendeleo ya Chama cha Ushirika yanategemea sana umadhubuti wa ushirikiano baina ya Wanachama, Bodi ya Uongozi na watendaji wa Chama katika utekelezaji wa wajibu wao. Ushirikiano huo unafungamanishwa na nguzo tatu ambazo ni: -

i. Umiliki wa Wanachama (Member Ownership)
ii. Udhibiti wa Wanachama (Member Control) na
iii. Ushiriki wa Wanachama (Member Participation)

Menejimenti (Watendaji) na Bodi ya Uongozi wanapaswa kila wakati kujenga mazingra ya kuwawezesha Wanachama kupiga hatua kuelekea kwenye nguzo hizo.

**Umiliki wa Wanachama**

Umuhimu wa Mwanachama ndani ya Chama chake unajidhihirisha pale ambapo Mwanachama ametimiza wajibu wake kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa Sheria na Masharti ya Chama.

Viashiria muhimu vya umiliki wa uanachama ni pamoja na uwiano wa hisa zake katika Chama dhidi ya mtaji wa nje ya Chama.

**Udhibiti wa Wanachama**

Udhibiti wa Wanachama huweza kudhihirika kupitia nyenzo mbalimbali ukiwemo mchakato wa kuandaa na kupitisha Masharti, Mipango na bajeti, Sera, Miongozo, maazimio ya Wanachama, Taarifa za maendeleo ya Chama zikiwemo taarifa za ukaguzi.

**Ushiriki wa Wanachama**

Nyenzo kuu za ushiriki wa wanachama ni kushirki na kushirikishwa katika shughuli za Chama, Mikutano, Fursa za kuhudumiwa na Chama na kupata Gawio (Dividends) kutokana na matokeo ya kazi yao ya pamoja.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 Kufanya ufuatiliaji na tathmini

Kazi ya ufuatiliaji na tathmini itafanywa na Wataalam kutoka Ofisi ya Mrajis, Mikoani na Wilaya/Halmashauri wakishirikiana kwa pamoja katika mchakato wa kutekeleza mpango na matokeo ya uhamasishaji wa Chama cha Ushirika kilichokusudiwa kuanzishwa au kuboreshwa na kutoa mrejesho wa hatua zote zilizochukuliwa. Aidha, Afisa Ushirika anatakiwa kufuatilia mara kwa mara juu ya maendeleo ya chama husika ili kutoa maelekezo na kuchukua hatua stahiki mapema pale inapohtajika.

Baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa ufuatiliaji na tathmini kwa chama kilichoanziswha ni pamoja na:

i. Kuanza kwa shughuli kuu ya kiuchumi ya Chama;
ii. Utoaji wa taarifa za maendeleo ya Chama; na
iii. Kufanyika kwa Mikutano ya Chama.

### 5.0 HITIMISHO

Mwongozo huu umeainisha mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika zoezi zima la uhamasishaji kwa mujibu wa mahitaji ya jamii hasa ikizingatiwa kwamba zipo aina nyingi za Vyama vya Ushirika vinavyoweza kuanzishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake.

Ni matarajio ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuwa Mwongozo huu utarahisisha kazi ya kuratibu majukumu ya uhamasishaji na usimamizi yanayotekelezwa na Wadau mbalimbali nchini. Aidha, watumiaji wanatakiwa kufanya rejea katika mwongozo huu ili kuhakikisha kwamba Vyama vya Ushirika vinaanzishwa na kuendeshwa kwa kuzingatia taratibu kama zilivyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni za vyama vya Ushirika.

# VIAMBATISHO

## 1. DHANA YA USHIRIKA

Mwananchi anapaswa kufahamu kwamba Ushirika una tafsiri mbili yaani Ushirika kama dhana na Ushirika kama taasisi.

### 1.1 Ushirika kama Dhana

Mhamasishaji anapaswa kuelewa dhana sahihi ya ushirika kabla ya kuingia katika jukumu la utoaji wa elimu na mafunzo ya ushirika (uhamasishaji). Baada ya kuelewa dhana hii mhamasishaji lazima aimiliki.

Dhana ya ushirika inajumuisha maeneo makuu matatu ambayo ni pamoja na *Maana ya Ushirika; Maadili ya Ushirika na Misingi ya Ushirika.*

### 1.2 Maana ya Ushirika

Ni muungano wa watu walioungana pamoja kwa hiari yao, kwa madhumuni ya kufanikisha mahitaji yao kwa kuazisha na kumiliki chombo chao kidemokrasia na kuchangia mtaji unaohitajika kwa usawa na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kutokana na shughuli zake ambazo wao hushiriki kikamilifu. Wanaoanzisha Ushirika hawana budi kuwa na mfungamano wa pamoja, mathalani wakulima wa zao Fulani, wakazi wa Kijiji au mtaa Fulani, mafundi, Waajiriwa n.k. Kwa mantiki hiyo Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali vinaweza kuanzishwa kulinanga na mahitaji ya walengwa.

### 1.3 Maadili ya Ushirika (Tunu za Ushirika)

Maadili ya UshirikaUshirika (Cooperative Values) yamejikita katika kujitegemea, Uwajibikaji, Demokrasia, Haki, Usawa na Mshikamano.

### 1.4 Misingi ya Ushirika

Uimara na ustawi wa ushirika unategemea sana uzingatiaji wa misingi ya kimataifa ya ushirika. Misingi ya Ushirika ni nguzo muhimu n ani lazima izingatiwe na mhamasishaji katika utoaji wa elimu na mafunzo ili kufikia malengo tarajiwa. Misingi hiyo ni Uanachama wa hiari na ulio wazi; Wanachama na Udhibiti wa Kidemokrasia; Ushiriki wa wanachama katika shughuli za kiuchumi;

Uhuru na kujitegemea; Elimu, Mafunzo na Taarifa; Ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Ushirika na Kuijali jamii.

## 1.5 Ushirika kama taasisi

Mhamasishaji anapaswa kuelewa dhana sahihi ya ushirika kama taasisi ili kuweza kuonesha utofauti wa ushirika kama dhana na ushirika kama taasisi. Baada ya kuelewa dhana hii mhamasishaji lazima aimiliki. Chama cha Ushirika ni taasisi/chombo kinachoundwa na wananchi kwa hiyari yao na kusajiliwa kwa mujibu wa sharia ya ushirika ili kukidhi mahitaji ya Wanachama. Nchini Tanzania Vyama vya Ushirika vinaundwa kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Ushirika iliyopo ambayo inahimiza kuundwa kwa Vyama vya Ushirika kwa kufuata DIRA inayoelekeza uwepo wa Vyama vya Ushirika imara na endelevu vyenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya Wanachama ya kiuchumi na kijamii. Sheria ya Vyama vya Ushirika imewekwa ili kutekeleza Sera hiyo.

## 2. AINA YA VYAMA VYA USHIRIKA VINAVYHOWEZA KUANZISHWA

Vyama vya Ushirika vinaweza kuanzishwa kulingana na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazofanyika na ambazo zinahitaji nguvu ya pamoja ili kuleta tija kwa wanachama wake na kuwafanya wamiliki bidhaa/mazao yao hadi wakati wa uuzaji ili kunufaika na matokeo ya kazi yao kupitia ushirika. Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Sheria ya Vyama vya Ushirika zimeweka misingi, taratibu na miongozo ya uanzishaji wa aina mbalimbali za Vyama vya Ushirika.

### 2.1 Ushirika wa Kilimo na Masoko (Agricultural Marketing Cooperative Society)

Hushughulika na aina mbalimbali za mazao ya kilimo katika uzalishaji, ununuzi, usindikajim uuzaji, usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo pamoja na mambo mengineyo yanayohusu shughuli za kilimo kadri itakavyokuwa imeainishwa katika Masharti ya Chama husika. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasipungua ishirini (20) na kuendelea.

### 2.2 Ushirika wa Akiba na Mikopo (Savings and Credit Cooperative Society-SACCOS):

Huu ni ushirika unaowezesha wanachama kujenga tabia ya kuweka akiba na baadae kukopeshana kwa masharti nafuu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo ni pamoja na ufugaji, kilimo, ujenzi wa majengo ya biashara, elimu, afya n.k. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua ishirikni (20) na kuendelea.

### 2.3 Ushirika wa Waalaji (Consumer Cooperative Society):

Hujihusisha na utoaji wa huduma zinazohitajika na wanachama, mathalani maduka ya vyakula, nguo, vifaa vya ujenzi, mashine za kusaga, kukoboa na kukamua nafaka n.k. kwa manufaa ya Wanachama wake na jamii kwa ujumla. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

**2.4 Ushirika wa Viwanda (Industrial Cooperative Society):**
Ushirika huu hulenga kwenye uanzishaji na uendeshaji wa viwanda vya aina mbalimbali kwa ajili ya kuongeza thamani. Mwanachama ni lazima awe na ujuzi/ufundi unaohitajika. Wanachama wa chama cha ushirika wa viwanda watakuwa ndio wafanyakazi wa kiwanda. Ushirika huu utaanxishwa na watu wasiopungua (10) na kuendelea.

**2.5 Ushirika wa Nyumba (Housing Cooperative Society):**
Ushirika huu huanzishwa kwa nia ya kuwawezesha Wanachama kupata makazi bora pamoja na majengo ya kibiashara. Pia ushirika wa aina hii unaweza kujielekeza katika kutoa huduma ya ujenzi, kumiliki mitambo pamoja na huduma za ushauri wa kitaalamu, ufundi, kutoa vifaa vya ujenzi au kujenga majengo ya kibiashara. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

**2.6 Ushirika wa Mifugo (livestock Cooperative Society):**
Ushirika huu huanzishwa ili kuwawezesha Wanachama kukidhi mahitaji yao yanayohusiana na shughuli za ufugaji pamoja na kupata soko bora la mazao ya mifugo. Ushirika huu unaweza kujihusisha pia na umiliki wa pamoja wa mifugo, majosho, uuzaji wa Ngozi, unenepeshaji na uchinjaji, usindikaji na uuzaji wa maziwa n.k. unaweza kuanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

**2.7 Ushirika wa Uvuvi (Fisheries Cooperative Society):**
Ushirika huu unalenga kujihusisha na shughuli za uvuvi, ufugaji wa samaki, upatikanaji wa zana bora za uvuvi, usindikaji wa samaki, utafutaji wa masoko n.k. Unaweza kuanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

**2.8 Ushirika wa Madini (Mining Cooperative Society):**
Madini ni zao lolote linalopatikana kwa kuchimbuliwa kutoka ardhini, mfano; madini ya vito, chuma, mchanga, mawe, kokoto, n.k. Ushirika huu unalenga kuunganisha wachimbaji wadogo wadogo na wa kati ili kuweza kufanya kazi zao kwa pamoja na kwa tija. Mathalani wachimbaji hawa wanaweza kupata umiliki wa maeneo makubwa kumudu kupata mikopo na mitambo ya kuchimba madini na soko la uhakika la madini. Usirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

**2.9 Ushirika wa Benki (Cooperative Bank):**

Benki za ushirika ni taasisi zinazoundwa na Wanaushirika ili kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti na riba nafuu. Uendeshaji wa vyombo hivi vya kifedha huongozwa na kusimamiwa na sheria mbili ambazo ni Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na Sheria ya benki na taasisi za fedha. Wanaushirika huanzisha benki za Ushirika kupitia Vyama vyao vya Ushirika kwa kuwekeza mitaji yao. Kigezo muhimu cha kuweza kusajili benki ni kukidhi matakwa ya Sheria ya benki pamoja na kukidhi mahitaji ya Wanachama yanayokusudiwa.

**2.10 Tanbihi:**

Kuna aina nyingi za Vyama vya Ushirika vinavyoweza kuanzishwa kulinanga na mahitaji ya wananchi na mazingira husika. Wananchi wanapaswa waelimishwe na kusaidiwa kuibua aina mbalimbali za Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kutumia fursa zinzowazunguka.

## 3. Wajibu na Haki ya Mwanachama

### 3.1 Wajibu

i. Kushiriki katika shughuli zote za kiuchumi zinazohusu chama chake.
ii. Kufuata Sera, Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama.
iii. Kulipa kiingilio, kununua hisa, kuweka akiba na amana pamoja na kulipa michango mingine itakayokubaliwa na Wanachama.
iv. Kulinda na kutetea mali za Chama pamoja na kulipa madeni.
v. Kushiriki katika Mikutano ya Chama na kufuata maamuzi yaliyotolewa.
vi. Kudhamini nakulipa mkopo alioudhamini endapo mdhaminiwa ameshindwa kurejesha mkopo huo.

### 3.2 Haki

i. Kusikilizwa
ii. Kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi.
iii. Kupiga kura na kupigiwa kura.
iv. Kuhoji na kupata taarifa zote zinazhusu Chama chake hususani taarifa za ukaguzi na taarifa nyingine muhimu.
v. Kupatiwa taarifa na kuarifiwa kuhusu masuala yote ya Chama.
vi. Kuhudhuria na kushiriki katika Mikutano Mikuu ya Chama.
vii. Kujitoa uanachama.
viii. Kukata rufaa.
ix. Kupata kipato na manufaa mengine yanayotokana na shughuli za biashara ya Chama.
x. Kuteua mrithi kufuatana na Masharti ya Chama.
xi. Kuitisha Mkutano kwa mujibu wa Kanuni na Masharti ya Chama.
xii. Kushiriki katika kuandaa na kurekebisha Masharti ya Chama.
xiii. Kupatiwa hati baada ya kukamilisha malipo yote ya hisa kwa mujibu wa Masharti ya Chama.
xiv. Kukopa katika Chama chake cha Ushirika kwa mujibu wa Masharti ya chama.

xv. Kukagua nyaraka (document) za Chama chake kwa mujibu wa masharti ya Chama.

4. Kudadisi uchumi katika Vyama vya Ushirika ("Viability Assessment Guide for Cooperative Society")

## PART I

### 1.0 INTRODUCTION:

1.1 Proposed Name.............................................
Region ............................District ......................

1.2 Area of operation ..................................................

1.3 Initial Members ....................................................

1.4 Potential Members ................................................

1.5 The nearest society is ............................ Km. away

## PART II

### 2.0 MEMBERSHIP QUALITY FACTORS

2.1 The common needs criterion
2.2 The common Bond criterion

## PART II

### 3.0 ECONOMIC DATA

3.1 Basic Initial Requirement for activity e.g. Building ....................
3.2 Source of Funds for activity ....................................
- Entrance Fee
- Share contributions
- Borrowed capital
- Others

3.3 Economic stability of Area where society will operate (trend of the economy in this area for the past several years and for several years to come).
3.4 Supply and Demand Analysis for ..................... Product (To show purchasing power and the needs for the product).
- Production capacity
- Availability of Raw Materials
3.5 Assessment of Income and Expenditure (To show Annual income from operations, Annual Expenditure, Surplus/deficit and Projections for the same)
3.6 Audited Balance Sheets/Statement of Affairs for the Amalgamating societies.

## PART IV

## 4.0 SUPPORTIVE SYSTEMS

4.1 Good and Reliable Service
- Extension experts
- Banking
- Police
- Insurance
- Postal Services
- Transport facilities-Distance to Union/Factory
- Storage facilities
- Processing facilities
- Availability of Manpower among the potential members

4.2 Government Support (i.e recognition form the Government/Party)
4.3 Support from other institutions/Organizations

## PART V

## 5.0 LIMITATIONS

5.1 Geographical environment
5.2 Business competition

## PART VI

**6.0 SOCIAL CONSIDERATIONS**

6.1 Social impact to members
6.2 Social impact to non-members
6.3 Social costs
6.4 Ability of society to educate its members

## PART VII

**7.0 RECOMMENDATIONS**

7.1 To give a general opinion regarding
- Business efficiency and effectiveness

7.2 To give advice to the Registrar regarding,
- Viability and suitability of Cooperative activities and the society in general for registration.